TANGAZO LA SERIKALI Na. 32 la Tarehe 17/1/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA), (SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))*

MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA HIFADHI YA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MLIMBA YA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 907 la 2023

**1.** Sheria Ndogo hii itajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba ya Mwaka 2023 ambayo hapa imerejewa kama “Sheria Ndogo kuu”.

Marekebisho ya aya ya 7

**2.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika aya ya 7 kwa kufuta na kuandika upya aya ndogo ya (4) kama ifuatavyo:

“(4) Kabla ya kuuza mfugo chini ya aya ndogo ya (3), Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mmiliki na umma kuhusu kusudio la kuuza mfugo huo.”.

Marekebisho ya aya ya 11

**3.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika aya ya 11(1)(a) kwa kuongeza maneno “na miinuko bila kufuata kanuni za kilimo,” mara baada ya neno “miteremko”.

Dodoma,
25 Machi, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri Wa Nchi- OR-TAMISEMI*